

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 38 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** APRILI 2024

MIKA MITATU YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI NI NEEMA KUBWA KWA TSC NA WALIMU

- ✦ Walimu 37,473 Waajiriwa
- ✦ Walimu 227,383 wapandishwa vyeo
- ✦ Walimu 20,436 wabadilishiwa muundo
- ✦ Ujenzi wa Jengo la Ofisi wafikia asilimia 37
- ✦ Kila Ofisi ya Wilaya yapatiwa pikipiki
- ✦ Komputa mpakato 159 zanunuliwa



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

RAIS SAMIA AENDELEE KUUNGWA MKONO ILI AZIDI KULETA MAGEUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU

Ni jambo lisilopingika kuwa katika kuadhimisha miaka mitatu (3) ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kumekuwa na mapinduzi makubwa katika Sekta ya Elimu jambo linaloweza elimu yetu kuendelea kuwa bora.

Mabadiliko katika Sekta ya Elimu yamegusa nyanjambalimbali ikiwemo walimu kutatuliwa changamoto mbalimbali za kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, kubadilishiwa vyeo, kuendelea kulipwa fedha za malimbikizo mishara na likizo, ujenzi wa nyumba za walimu, ukarabati na ujenzi wa madarasa na shule pamoja na ujenzi wa maabara.

Vilevile, Serikali ya Rais Samia itaendelea kukumbukwa kwa uamuzi wake wa kuandaa Sera na Mtaala mpya wa elimu jambo ambalo

linaongeza fursa za wanafunzi katika soko la ajira pale wanapohitimu elimu zao.

Tunaamini kuwa Rais Samia bado ana malengo makubwa katika kuendelea kuboresha elimu ya Tanzania, na hii imethibitishwa kwa namna ambavyo anaendelea kutafuta fedha ndani na nje ya nchi huku fedha nyingi zikielekezwa katika Sekta ya Elimu.

Nimuhimu kila mmoja kuendelea kumuunga mkono Rais Samia ili tuendeleo kushuhudia mabadiliko zaidi ya maendeleo katika Sekta hii muhimu. Hongera sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa uchapakazi wako uliotukuka. Walimu wana imani kubwa na wewe na wataendelea kukuunga mkono ili yale yote uliyopanga yafanyike katika Sekta ya Elimu yaweze kutimia kwa ajili ya Ustawi wa Watanzania Wote.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania




[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Miaka 3
YA SAMIA



Asante Rais
Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan

Mradi wa ujenzi wa Jengo la
Ofisi TSC Makao Makuu
unaendelea



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI NI NEEMA KUBWA KWA TSC NA WALIMU

Na Mwandsihi Wetu - Dodoma

Katika kuadhimisha miaka mitatu (3) ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan toka aingie madarakani, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inakiri kupata mafanikio mbalimbali yanayochangia kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Elimu.

Maendeleo haya katika Sekta ya Elimu ni matokeo ya dhamira ya dhati ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha walimu wanasimamiwa vizuri, wanatatuliwa changamoto zao na wanapata mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma bora kwa wanafunzi.

Kabla ya kufafanua mafanikio mbalimbali ambayo TSC imeyapata chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ni vyema tukumbushane juu ya TSC yenyewe, majukumu yake na inafanyaje kazi katika kuwahudumia walimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma, Tanzania Bara, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015.

TSC inatekeleza majukumu yake kupitia Ofisi ya Makao Makuu iliyopo mtaa wa Mtendeni jijini Dodoma pamoja na ofisi 139 zilizopo katika kila Wilaya Tanzania Bara.

Miongoni mwa majukumu ya TSC ni kusimamia masuala yanayohusu ajira ya Mwalimu



Sehemu ya pikipiki 63 na kompyuta mpakato 159 zilizokabidhiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohammed Mchengerwa (Mb) kwa TSC Novemba 27, 2023 katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Tambaza Jijini Dar es Salam.

ambayo ni kusajili na kutoa barua za ajira rasmi; kuthibitisha kazini; kupandisha vyeo; kubadilisha kazi/cheo waliojiendeleza; kuandaa Tange, kupitisha na kuratibu maombi ya kuajiriwa upya kwenye Utumishi wa Umma.

TSC pia inawajibika kushughulikia mafao ya wastaafu na mirathi ambayo haishughulikiwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kukokotoa mafao na kuwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hazina kwa ajili ya uhakiki na malipo. Jukumu lingine ni kusimamia Maadili na Nidhamu kwa Walimu kwa kuwaelimisha na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanaokiuka Sheria, Kanuni

na Maadili ya Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Tume hiyo inasimamia walimu 273,021 ambao kati ya hao, Walimu 181,149 ni wa Shule za Msingi na 91,872 ni wa Shule za Sekondari.

Katika kipindi cha miaka mitatu (3) tangu Rais Samia alipoingia madarakani, TSC imeendelea kupata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa kutoa huduma kwa walimu ambapo Walimu 37,473 walijajiriwa na kusajiliwa, 25,161 walithibitishwa kazini, Walimu 227,383 walipandishwa vyeo, 20,436 walibadilishwa miundo baada ya kujiendeleza na Walimu 6,937

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI NI NEEMA KUBWA KWA TSC NA WALIMU

walipewa vibali vya kustaafu.

Pia, TSC ilifanya kazi ya kukusanya, kuchambua na kuandaa taarifa ya tathmini ya usambazaji na uwiano wa walimu kupitia mfumo wa School Information System (SIS).

Aidha, TSC kwa kushirikiana na Ofisi ya Ras – UTUMISHI, OR – TAMISEMI na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini imefanikiwa kufanya uchambuzi wa walimu wote ili kubaini wenye changamoto za masuala ya kiutumishi ambapo hatua stahiki zinaendelea kuchukuliwa ili kila mwalimu mwenye madai ya msingi apatiwe haki yake.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia, TSC imefanikiwa kujenga Mfumo wa Kielektroniki wa Teacher's Service Management Information System (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma kwa walimu. Mfumo tayari umeanza kutumika na unalenga kurahisisha utoaji wa huduma katika masuala mbalimbali

ikiwemo kushughulikia Mashauri ya Nidhamu, Rufaa, Malalamiko, Mafao ya Ajira ya Mkataba na Mirathi na Pensheni ya kabla ya tarehe 1 Julai, 2004, Usajili wa Walimu na kutunza taarifa za wageni.

Sambamba na hayo, Rais Samia ameiwezesha TSC kufanya jumla ya mikutano ya Tume 11; Kamati za Wilaya 139 zilifanya vikao vya kisheria 1,390; jumla ya wateja 13,720 walifika ofisini na kupata huduma zihusuzo masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu yakiwemo ajira, mirathi, mikataba, mashauri ya nidhamu na mafao.

Aidha, jumla ya malalamiko 5,493 yalipokelewa na kushughulikiwa. Malalamiko hayo yalijumuisha kupandishwa vyeo, kubadilishiwa cheo, kuthibitishwa kazini, mashauri ya nidhamu na masuala ya mafao. Tume iliratibu kikao cha Wadau (OR – Ikulu, OR – UTUMISHI, OR – TAMISEMI, CAG, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa

Serikali, Wizara ya Elimu na PSSSF) kujadili changamoto mbalimbali kuhusu Utumishi wa Walimu na kutafuta ufumbuzi wa pamoja kama Serikali.

Pamoja na hayo, Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kushirikiana na Mradi wa World Vision Tanzania (WVT) waliandaa kitabu kinachotumika kufundishia Wakufunzi ngazi ya Wilaya kwenye maeneo ambako WVT wanaendesha shughuli zao. Ki tabu hicho kina mada mbalimbali zinazohusu Ajira, Maadili na Maendeleo ya Mwalimu.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Tume imetoa uamuzi wa rufaa 340. Katika usimamizi wa maadili ya walimu nchini mashauri ya walimu 3,206 yalitolewa uamuzi.

Chini ya usimamizi na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, TSC imeandaa Mwongozo kwa ajili ya kuwasidia Wakuu wa Shule kwa nafasi zao za Mamlaka za Nidhamu ngazi ya Shule kumesaidia kushughulikia masuala ya walimu ngazi ya shule na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa walimu.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, Tume imeanza ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu kupitia kwa Mkandarasi SUMA JKT katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma. Hadi kufikia tarehe 04 Februari, 2024 maendeleo ya ujenzi yanakadiriwa kufikia asilimia 37.

Pamoja na hayo, Rais Samia ameiwezesha TSC kusimika miundombinu ya mtandao wa intaneti (network Infrastructure) kwenye Ofisi za Wilaya katika Mikoa minne (4) ya Dodoma,



Hatua iliyofikiwa katika mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu hadi kufikia mwezi Machi, 2024.

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI NI NEEMA KUBWA KWA TSC NA WALIMU

Iringa, Dar es Salaam na Mwanza pamoja na Wilaya ya Kishapu na Morogoro ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2024 mtandao wa intaneti unapatikana kwenye Ofisi za Wilaya katika Mikoa hiyo.

Ukweli ni kwamba hatuwezi kuainisha mafanikio yote ya TSC yaliyotokana na uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan lakini jambo lingine ambalo litaendelea kukumbukwa ni kuiwezesha TSC kufanya utafiti kuhusu kujitathmini iwapo imeweza kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448.

Utafiti huo ulifanyika ambapo jumla ya wahojiwa 788 walihojiwa wakijumuisha walimu, Maofisa Elimu, Wananchi, Asasi za Kiraia, Waandishi wa Habari, Wabunge, Maofisa kutoka Wizara ya Elimu na OR - TAMISEMI. Utafiti huo ulifanyika kwenye Wilaya 22 katika Mikoa saba (7) ya Tanzania Bara.

Taarifa ya Utafiti huo inaonesha kuwa kati ya majukumu kumi na moja (11) ambayo Tume ilikabidhiwa kwa mujibu wa Sheria Sura 448, yapo majukumu ambayo Tume imeyatekeleza kwa asilimia zaidi ya 50.

Rais Samia ameiweka TSC kuwa miongoni mwa watekelezaji wa shughuli za mradi wa BOOST katika kipengele cha Shule salama na usimamizi wa Walimu.

Kazi zilizotekelezwa katika mradi huo ni kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu, kuwajengea watumishi wa Tume uwezo katika kutekeleza majukumu ya Tume kwa kununua



Walimu wa Shule ya Sekondari Dodoma pamoja na wataalamu wa Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) wakifuatilia wasilisho la mada kutoka kwa Afisa TEHAMA wa TSC, Pastory Munyaki (hayupo pichani) kuhusu namna ya kujisajili na kuingiza taarifa katika mfumo huo Novemba 2, 2023.

laptops 159, kugawa vishikwambi 550 kwa watumishi na vifaa vingine vya TEHAMA na samani za ofisi.

Rais Samia ameiwezesha TSC kununua pikipiki 136 kwa ajili ya ofisi za Wilaya na kufanya kila Wilaya kupata kifaa hicho cha usafiri. Pikipiki hizo zimesaidia kwa kiasi kikubwa watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kuwafikia walimu na kutatua changamoto mbalimbali kwa wakati.

Rais Samia Suluhu Hassan amefanya mengi makubwa katika kuboresha mazingira ya elimu nchini. Rais amefanikiwa kushughulikia malamiko mbalimbali ya walimu ikiwemo kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu, vilevile Rais Samia ameboresha mazingira

ya kufundishia kwa kuongeza vyumba vya madarasa, ununuzi wa vitabu, ujenzi wa maabara pamoja na ukarabati na ujenzi wa shule na nyumba za walimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu inaungana na wataanzania wote kumshukuru na kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo makubwa anayoyaleta katika Taifa letu. Hivyo ni wajibu kwa kila mtumishi wa umma na kila mtanzania kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, weledi na nidhamu ili Tanzania iendelee kuwa na ustawi bora zaidi. Hongera sana Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Walimu wana imani kubwa na wewe na wataendelea kukuunga mkono, kazi iendelee.

MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN MADARAKANI NI NEEMA KUBWA KWA TSC NA WALIMU



Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa sasa Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki akibonyeza kitufe kuzindua Mfumo wa Kielektroniki wa Tume (TSCMIS) katika Ukumbi wa Matokeo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi jijini Dodoma Machi 16, 2023.



Ukaguzi wa Miundombinu ya mtandao wa intaneti iliyosimikwa katika ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Iringa ukiwa unafanyika.

ZIARA YA TSC UKEREWI KATIKA KATA YA MURITI

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Stephen Kushoka akijibu maswali mbalimbali kutoka kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari katika Kata ya Muriti wakati wa ziara ya TSC Wilaya ya Ukerewe iliyofanyika katika Kata hiyo Machi 23, 2024.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ukerewe, Mwl. Magreth David akitoa elimu juu ya Maadili katika Utumishi wa Walimu kwa walimu wa shule za Msingi na Sekondari katika Kata ya Muriti wakati wa ziara ya TSC Wilaya ya Ukerewe iliyofanyika katika Kata hiyo Machi 23, 2024.

Baadhi ya walimu wa kata ya Muriti wakisikiliza maada mbalimbali zilizofundishwa na watendaji kutoka ofisi ya TSC Wilaya ya Ukerewe Machi 23, 2024.



SERIKALI YAONGEZA TAHASUSI 49, WAHITIMU KIDATO CHA NNE WAPEWA FURSA KUFANYA MACHAGUO UPYA

**Na Mwandishi wetu –
Dar es Salaam.**

Serikali imeongeza Tahasusi (combination) mpya 49 kutoka 16 zilizokuwepo awali kwa wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano kuanzia mwezi Julai, 2024.

Kuongezeka kwa Tahasusi hizo mpya kunafanya kuwepo kwa Jumla ya Tahasusi 65 na hivyo kutoa wigo mpana wa uchaguzi kwa wanafunzi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2024 Toleo la mwaka 2023.

Tahasusi hizo zipo katika makundi saba (7) ambayo ni Tahasusi za Sayansi ya Jamii, Lugha, Masomo ya Biashara, Sayansi, Michezo, Sanaa, na Tahasusi za Elimu ya Dini.

Kufuatia mabadiliko hayo, Wahitimu wa Kidato cha Nne mwaka 2023 wameagizwa kufanya mabadiliko ya Tahasusi za kidato cha Tano na kozi za vyuo kwa njia ya mtandao kwenye mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi wa kidato cha Tano na vyuo mwaka 2024.

Taarifa hizo zilibainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa alipokutana na waandishi wa habari Machi 20, 2024 jijini Dar es Salaam amapo alieleza kuwa TAMISEMI imekamilisha zoezi la awali la kuingiza kwenye kanzidata taarifa zilizo kwenye Fomu za Uchaguzi za wanafunzi kama zilivyojazwa na wanafunzi wakiwa shuleni.

"Napenda mtambue kuwa Mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu kwa Kidato cha Tano yameanza kutekelezwa, ambapo utekelezaji



huo umehusisha uanzishaji wa Tahasusi mpya 49, kutoka 16 zilizokuwepo awali hadi kufikia tahasusi 65.

"Kukamilika kwa zoezi hili kunatoa fursa kwa wanafunzi kuweza kufanya mabadiliko ya machaguo/ tahasusi/ kozi kwa njia ya mtandao (online). Baada ya wanafunzi kufanya marekebisho yao, kanzidata hiyo ndiyo itakayotumika kuwachagua na kuwapangia nafasi za Kidato cha Tano na Kozi mbalimbali katika Vyuo vya Kati na vya Elimu ya Ufundi kwa kuzingatia sifa za ufaulu na machaguo yao," alisema Mchengerwa.

Amebainisha kuwa, zoezi la kubadilisha tahasusi na vyuo limeanza rasmi leo Machi 20 hadi Aprili 30, 2024 huku akitoa wito kwa Wanafunzi, wazazi na walezi kushauriana kikamilifu ikiwa ni pamoja na kupata ushauri wa kitaalam na kitaaluma kabla ya kufanya mabadiliko ya tahasusi au Kozi.

Amefafanua kuwa, Serikali imekuwa ikitoa fursa kwa wahitimu wa Kidato cha Nne kufanya mabadiliko ya machaguo ya Tahasusi na Kozi mbalimbali walizozichagua kupitia Fomu ya Uchaguzi (Selfform).

"Fursa hii huwawezesha wanafunzi kurekebisha

machaguo yao kulingana na ufaulu waliopata kwenye matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA).

"Kwahiyo Ofisi ya Rais TAMISEMI inatoa fursa kwa wahitimu wa Elimu ya Sekondari Kidato cha Nne mwaka 2023 kubadili machaguo yao ili kutoa nafasi zaidi kwa Mwanafunzi kusoma tahasusi au kozi itakayomwandaa kuwa na utalam stahiki katika maisha yake ya baadaye. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wakati wa ujazaji wa fomu za machaguo ya awali, tahasusi mpya 49 hazikuwepo kwenye orodha ya machaguo na pia matokeo ya mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne hayakuwa yametoka kumuwezesha mwanafunzi kuweza kuwa na machaguo mazuri zaidi kulingana na ufaulu wake," alisema.

Ameongeza kuwa, zoezi hilo litatoa fursa zaidi ya wanafunzi kuongeza machaguo na kufanya machaguo mapya ya Tahasusi na Kozi.

"Kwa umuhimu huo, wahitimu wote wanahimizwa kufanya marekebisho ya machaguo ya tahasusi na kozi kulingana na ufaulu wao, kwa kuingia kwenye Mfumo wa Uchaguzi wa Wanafunzi (Student Selection MIS) unaopatikana kupitia kiungan cha selfform.tamisemi.go.tz.

"Aidha, maelekezo kwa wahitimu na jinsi ya kufanya mabadiliko yanapatikana kwenye mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi. Ili kuingia kwenye mfumo itabidi mhitimu atumie namba ya mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne mwaka 2023, jina lake la mwisho, mwaka wa kuzaliwa na alama ya ufaulu aliyopata kwenye somo atakaloulizwa na mfumo au swali lolote atakaloulizwa," amesisitiza.



UJUMBE KUTOKA KWA WANAWAKE WAKUU WA TAASISI/MASHIRIKA NA VYUO VYA UMMA

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI TAREHE 8.3.2024



Paulina M. Nkwama

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu
Ofisi ya Rais TAMISEMI

“

“Elimu ndio msingi wa Maendeleo kwa mtu mmoja moja, jamii na Taifa kwa ujumla. Utoaji wa Elimu kwa usawa kati ya wanawake na wanaume unatufanya sote kusafiri pamoja katika safari yetu ya kufikia maendeleo. Ninawaomba wataanzania wote tushirikiane kuhakikisha tunatoa fursa sawa ya elimu kwa watoto wa kike na wa kiume. Tukumbuke, ukimwelimisha Mwanamke, umeelimisha jamii nzima. Tutaendelea kusimamia walimu ndani ili waendeleo kutoa elimu kwa usawa kwa wanafunzi wetu bila kuwa na ubaguzi wa kijinsia.”

”

Majukumu yanayosimamiwa na taasisi

- Kuendeleza na kusimamia Utumishi wa Walimu;
- Kuajiri, kupandisha vyeeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
- Kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa Walimu ndani ya Serikali za Mitaa na Shule;
- Kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya Mamlaka ya Nidhamu;
- Kutunza daffari la kumbukumbu za walimu wote waliopo kwenye Utumishi wa Umma;
- Kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
- Kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu Utumishi wa walimu na kumshauri Waziri inavyostahiki;
- Kutathmini hali ya Walimu na kushauri Waziri yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu ndani;
- Kuandaa Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi ya mwalimu;
- Kufanya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Waziri linafaa au kutegemewa katika utekelezaji bora wa kazi za Tume.

Imedhaminiwa na:



COSOTA
CHAMA CHA TUMUISHI TANZANIA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**ORODHA YA TAHASUSI ZA KIDATO CHA TANO ZITAKAZOTUMIKA
KUANZIA MWEZI JULY, 2024**

Na.	MASOMO
	A: TAHASUSI ZA SAYANSI YA JAMII
1	History, Geography and Kiswahili (HGK)
2	History, Geography and English Language (HGL)
3	History, Geography and French (HGF)
4	History, Kiswahili and English Language (HKL)
5	History, Geography and Arabic (HGA _r)
6	History, Geography and Chinese (HGCh)
7	History, Geography and Economics (HGE)
8	History, Geography and Fasihi ya Kiswahili (HGFa)
9	History, Geography and Literature in English (HGLi)
	B: TAHASUSI ZA LUGHA
10	Kiswahili, English Language and French (KLF)
11	Kiswahili, English Language and Arabic (KLA _r)
12	Kiswahili, English Language and Chinese (KLCh)
13	Kiswahili, Arabic and Chinese (KA _r Ch)
14	Kiswahili, Arabic and French (KA _r F)

15	English Language, French and Arabic (LFAr)
16	English Language, French and Chinese (LFCh)
17	French, Arabic and Chinese (FArCh)
18	History, English Language and French (HLF)
19	History, English Language and Arabic (HLAr)
20	History, English Language and Chinese (HLCh)
C: TAHASUSI ZA MASOMO YA BIASHARA	
21	Economics, Business Studies and Accountancy (EBuAc)
22	Economics, Geography and Mathematics (EGM)
23	Economics, Commerce and Accountancy (ECAc)
24	Economics, Computer Science and Mathematics (ECsM)
25	Business Studies, Accountancy and Computer Science (BuAcCs)
26	Business Studies, Accountancy and Mathematics (BuAcM)
27	Economics, Business Studies and Islamic Knowledge (EBuI)
D: TAHASUSI ZA SAYANSI	
28	Physics, Chemistry and Mathematics (PCM)
29	Physics, Chemistry and Biology (PCB)
30	Physics, Geography and Mathematics (PGM)
31	Chemistry, Biology and Geography (CBG)
32	Physics, Mathematics and Computer Science (PMCs)
33	Chemistry, Biology and Agriculture (CBA)
34	Chemistry, Biology and Food and Human Nutrition (CBN)

	E: TAHASUSI ZA MICHEZO
35	Biology, Food and Human Nutrition and Sports (BNS)
36	English Language, Music and Sports (LMS)
37	Kiswahili, Music and Sports (KMS)
38	Fasihi ya Kiswahili, Music and Sports (FaMS)
39	Literature in English, Music and Sports (LiMS)
40	French, Music and Sports (FMS)
41	Arabic, Music and Sports (ArMS)
	F: TAHASUSI ZA SANAA
42	Kiswahili, English Language and Theatre Arts G(KLT)
43	Kiswahili, French and Theatre Arts (KFT)
44	Fasihi ya Kiswahili, English Language and Theatre Arts (FaLT)
45	Kiswahili, Literature in English and Theatre Arts (KLiT)
46	Kiswahili, English Language and Music (KLM)
47	Kiswahili, French and Music (KFM)
48	Fasihi ya Kiswahili, English Language and Music (FaLM)
49	Kiswahili, Literature in English and Music (KLiM)
50	Kiswahili, English Language and Fine Art (KLFi)

51	Kiswahili, French and Fine Art (KFFi)
52	Fasihi ya Kiswahili, English Language and Fine Art (FaLFi)
53	Kiswahili, Literature in English and Fine Art (KLiFi)
54	Kiswahili, Textile and Garment Construction and Fine Art (KTeFi)
55	English Language, Textile and Garment Construction and Fine Art (LTeFi)
56	Arabic, Textile and Garment Construction and Fine Art (ArTeFi)
57	Chinese, Textile and Garment Construction and Fine Art (ChiTeFi)
G: TAHASUSI ZA ELIMU YA DINI	
58	Islamic Knowledge, History and Geography (IHG)
59	Divinity, History and Geography (DHG)
60	Islamic Knowledge, History and Arabic (IHAr)
61	Divinity, History and English Language (DHL)
62	Islamic Knowledge, History and English Language (IHL)
63	Divinity, History and Kiswahili (DHK)
64	Islamic Knowledge, History and Kiswahili (IHK)
65	Divinity, Kiswahili and English Language (DKL)

MRADI UJENZI WA OFISI ZA TSC

Hatua iliyofikiwa katika mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu hadi kufikia mwezi Machi, 2024.



MRADI UJENZI WA OFISI ZA TSC

Hatua iliyofikiwa katika mradi wa Ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu hadi kufikia mwezi Machi, 2024.





OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Pongezi

Menejimenti na Watumishi wa
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
Tunakupongeza kwa kuteuliwa kuwa
Naibu Waziri, Ofisi ya Rais -TAMISEMI

Tunaahidi kukupa ushirikiano
katika kutekeleza majukumu yako



Mhe. Zainab Athuman Katimba



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Shukrani

Menejimenti na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Tunakushukuru kwa kipindi chote ulichotumikia Ofisi hii kama Naibu Waziri (Elimu) ambapo kwa pamoja tumeweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Pia tunakupongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Tunakutakia kheri katika majukumu yako mapya



Mhe. Deogratius Ndejemi



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Menejimenti na Watumishi wa
Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
wanawatakia Watanzania wote

PASAKA

Njema

'Tusherehekee kwa Amani'



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC BABATI YATOA ELIMU SHULENI

Na Mwandishi wetu – Babati.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Babati imefanya ziara katika shule za Sekondari za Sigino, Kwang na Shule ya Msingi Haysam kwa lengo la kutoa elimu juu ya Masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu. Ziara hiyo ilifanyika mwezi Machi, 2024.



DKT. BITEKO ATAKA UWEKEZAJI KWENYE ELIMU UMGUSE MWALIMU



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko akizindua krogramu ya kuboresha kada ya Ualimu nchini (GPETSP) katika ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam tarehe 13 Machi, 2024.

Na. Mwandishi wetu – Dar es Salaam.

Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema uwekezaji unaofanywa katika Sekta ya Elimu ni lazima umguse mwalimu kwani ndiye mwenye dhamana na masuala yaliyopo kwenye mfumo wa elimu.

Mhe. Biteko aliyasema hayo Machi 13, 2024 katika Ukumbi wa Diamond Jubilee Jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuzindua Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu inayolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

“Mwalimu ndiye rasilimali kuu inayofanya rasilimali nyingine ziweze kuleta matokeo chanya kwenye Sekta ya Elimu, ndio

maana programu tunayoizindua leo inaonesha kwa vitendo kuwa Serikali tunatambua kwamba lazima tuwekeze zaidi kwenye mazingira ya kujifunzia na kufundishia lakini pia kuwatambua walimu kuwa ndio watu tunaowategemea kufanya elimu yetu iweze kwenda mbele” Alisema Mhe. Dkt. Biteko.

Akimwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema, Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya jitihada za makusudi ili masuala yanayowahusu walimu nchini yafanyiwe kazi ili kuwapunguzia changamoto zinazowakabili kwa lengo la kufanya wanafunzi wapate elimu bora.

Aidha, Dkt. Biteko alisema Serikali inaendelea kufanya maboresha ya bajeti ya Elimu kwani kwa mwaka 2021 jumla ya

shilingi Trilioni 4.7 zilitolewa na kuongezeka hadi shilingi Trilioni 5.7 sawa na asilimia 20.4 mwaka 2023.

Kuhusu ufaulu alisema kutokana na kazi nzuri ya walimu kote nchini, wamewezesha kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa shule za msingi kwenda sekondari kutoka 907,802 mwaka 2021 hadi 1,092,984 mwaka 2023 ikiwa ni ongezeko la asilimia 20.4 sambamba na kuwapandisha vyeo walimu 227,383 pamoja na kuwabadilishia vyeo walimu 20

Dkt. Biteko ametoa maagizo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuangalia utaratibu mzuri wa kuwapa motisha walimu mfano kutenga walau siku moja ya kuwapa motisha walimu badala ya kusubiri Mei Mosi ya kila mwaka lengo likiwa ni kupata matokeo bora kwa wanafunzi.

DKT. BITEKO ATAKA UWEKEZAJI KWENYE ELIMU UMGUSE MWALIMU



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko akizungumza wakati wa hafla ya kuzindua Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu nchini (GPETSP) katika Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam tarehe 13 Machi 2024.

Akitoa maelezo ya awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika wa Elimu Duniani (GPE) ambaye pia ni Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete alisema Mfuko wa GPE umeshachangia Dola za Marekani milioni 330 nchini Tanzania na kwamba GPE inaunga mkono juhudi za Serikali kuboresha Sekta ya Elimu ili kila mtoto awe na ujuzi na maarifa na sasa Taasisi hiyo imeidhinisha ufadhili wa Dola za Marekani milioni 80 kwa ajili ya programu.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda alisema kuwa, programu iliyozinduliwa ya Kuboresha Kada ya Ualimu (GPE TSP) inagusa sehemu mbalimbali katika Kada ya Ualimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha utoshelevu wa walimu, kutoa walimu bora, uwepo wa miundombinu, vitendea kazi, kuendeleza makazi ya walimu na motisha kwa walimu ijapokuwa Serikali inatekeleza

haya nao GPE inakuja kuongeza nguvu na kasi ya utekelezaji wa programu za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu.

Naye Charlotta Ozaki Macias Balozi wa Sweeden nchini Tanzania alisema Washirika

wa Elimu Duniani (GPE) wataendeleza ushirikiano na Tanzania ili kuhakikisha Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu inafanikiwa na kusema kuwa awamu ya tatu ya ufadhili inawalenga zaidi walimu kwa ajili ya kuwaweka mazingira wezeshi na endelevu ili kutoa elimu bora kwani haki ya kupata elimu ni haki ya kila mtoto.

Kwa upande wake aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI (ELIMU), Deogratius Ndejemi, alimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza katika Sekta ya Elimu kwani uwekezaji alioufanya umeleta tija kwa kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji lakini pia aliahidi kuendelea kusimamia masuala ya elimu nchini pamoja na mitaala na Sera iliyobereshwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dkt. Doto Biteko pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Kimataifa inayoshughulikia Masuala ya Elimu Duniani (GPE), Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakiwa katika hali ya furaha wakati wa uzinduzi wa Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu nchini (GPETSP) katika Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam tarehe 13 Machi 2024.

TSC MISSENYI YATOA ELIMU KWA WALIMU KATA YA NSUNGA



Na Mwandishi wetu – Missenyi.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Missenyi imetoa mafunzo elekezi juu ya Maadili na Utendaji bora wa kazi ya ualimu kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Kata ya Nsunga wilayani humo. Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni na kuhudhuriwa na viongozi wa Kata hiyo akiwemo Diwani, Afisa Elimu Kata pamoja na Mtendaji Kata.



WALIMU MSIKATISHWE TAMAA, SERIKALI INASHUGHULIKIA HOJA ZENU: DKT. MSONDE

**Na Mwandishi wetu –
Kilimanjaro.**

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu Dkt. Charles Msonde ametoa wito kwa walimu kuendelea kufanya kazi na kutokukatishwa tamaa na baadhi ya watu akiwaeleza Serikali itaendelea kuhakikisha haki na hadhi ya walimu inalindwa.

Hayo aliyasema katika kikao alichokaa na walimu wa shule za sekondari na msingi wa Halmashauri ya Wilaya Moshi tarehe 19 Machi, 2024 katika Shule

ya Sekonadari Weruweru mkoani Kilimanjaro.

“Ninyi ni wasaidizi wa Mhe. Rais katika eneo la elimu na anawaamini sana, ni muhimu kwa kila mmoja wetu kufanya kazi kwa bidiii, weledi na uzalendo ili kuwasaidia wanafunzi kupata elimu bora kwa maendeleo ya Taifa letu,” alisema Dkt. Msonde

Dkt. Msonde alisema Serikali imeendelea kushughulikia changamoto za walimu zikiwemo kupandishwa madaraja, kubadilishiwa cheo (recategorization), madai ya uhamisho, malipo ya fedha za likizo, malimbikizo ya mshahara, na kuwashughulikia wale wote wanatoa kauli zisizoridhisha kwa

watu wanaowahudumia walimu.

Alisema changamoto hizo zimeendelea kushughulikiwa na kuhusu kupandishwa kwa madaraja maafisa utumishi wa mikoa na halmashauri walihakiki taarifa za mwalimu mmoja mmoja ambapo taarifa za walimu 278,000 zimehakikiwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais - UTUMISHI.

Naye Mwl. Ackbaru Hema aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya walimu hasa yale Naibu Katibu Mkuu Elimu aliyoyasema ambayo ndio kilio kikubwa. Amesema wataendela kufanya kazi kwa uadilifu na kuhakikisha elimu ya watoto wa Tanzania inakuwa bora.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu Dkt. Charles Msonde akizungumza na Walimu katika Wilayani Mwangi mkoani Kilimanjaro hivi karibuni.

SERIKALI YASISITIZA WALIMU KUFANYA MITIHANI KABLA YA KUAJIRIWA

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesisitiza kuwa katika kutekeleza mitaala mipya ya elimu, walimu wapya watafanya mtihani kabla ya kuajiriwa na watakaofanya vizuri ndio watakaopata nafasi.

Waziri Mkenda, alisema hayo Machi 7, 2024 alipokutana na wahariri na waandishi wa habari kuelezea sera na mitaala mipya ya elimu na mafanikio katika sekta ya elimu kwa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Alisema mpango huo utasaidia kupata walimu wenye uwezo zaidi kutokana na idadi ya wanaoomba ajira hiyo kuwa kubwa huku

akiweka wazi kuwa utaratibu wa mitihani kwa watumishi kabla ya kuajiriwa, kwa mujibu wa serikali, ni jambo la kawaida katika kada mbalimbali.

Prof. Mkenda ameongeza kuwa utaratibu huo utasaidia kuondoa lawama kwa baadhi ya watu wanaofikiri ajira za walimu zinatolewa kwa upendeleo.

"Sasa hivi walimu ni wengi kwa hiyo ukitangaza ajira hapa ni vita. Watu wakisikia ajira zimetangazwa kila mtu anaomba msaada binafsi ana mtu wake. Sasa tukisema kigezo gani kitumike kama wameomba 10,000, tunahitaji 2,000 tunachagua hawa," alisema.

Aliongeza kuwa, "kutokoana na changamoto hiyo, tukaona tuweke utaratibu wa kuwafanyia

uthamini kuwapa mitihani na watakaofaulu wataajiriwa. Ukiona umekosa, unaweza kukata rufani ili mtihani wako usahihishwe tena. Hii itaondoa kelele za mbunge wa jimbo fulani kuulizwa ajira za walimu" alisisitiza.

Hata hivyo, Prof. Mkenda alisema utaratibu huo hautawahusu walimu walioko kazini kwa sasa ambao wao wataendelea kupewa mafunzo ya mara kwa mara ili kuondokana na changamoto katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 214 Toleo la 2023 na mitaala mipya.

Kuhusu sera ya elimu na mitaala mipya alisema kwa mwaka huu imeanza mitaala mipya kwa kwa elimu ya awali, darasa la kwanza na la tatu, elimu ya sekondari kidato cha kwanza kwa shule zenye mkondo wa amali, vyuo vya elimu na kidato cha tano.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)